

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO



UTARATIBU WA MAOMBI YA KUBADILI MATUMIZI

Utaratibu wa kubadili matumizi unafanyika chini ya sheria Na. 8 ya Mipango Miji ya Mwaka 2007.

Hatua ya kwanza ni kuwasilisha barua ya maombi iliyosainiwa na mmiliki wa kiwanja ikieleza mambo yafuatayo:

1. Matumizi yaliyopo
2. Matumizi anayoomba
3. Sababu za kubadili matumizi

VIAMBATANISHO

Maombi ya mabadiliko ya matumizi yanawasilishwa yakiwa na majalada matatu yenye viambatanisho vifuatavyo:

1. Nakala za nyaraka za umiliki, hati au barua ya toleo
2. Ramani ya upimaji
3. Mchoro wa mipangomiji
4. Michoro ya uendelezaji au ujenzi anaokusudia
5. Nakala za Risiti za kodi ya majengo kwa kiwanja kilichoendelezwa
6. Nakala za Risiti ya kodi ya ardhi

HATUA

1. Kubandika bango la kusudio la kubadili matumizi kwa kipindi cha siku 30
2. Ukaguzi wa eneo

3. Kuandaa taarifa ya kitaalamu
4. Kuwasilishwa taarifa ya kitaalamu kwenye kikao cha kamati ya Mipangomiji na mazingira kwa ajili ya kujadiliwa
5. Kuwasilisha taarifa ya kitaalamu pamoja na muhtasari wa kikao Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa
6. Kuwasilisha Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kupata idhini